



*Taarifa kwa Umma, Jumatatu 7 Februari 2011*

## **Kuweka wazi vitabu vya bajeti!**

Serikali kuweka wazi vitabu vya bajeti kwa wananchi na wabunge ni jambo muhimu katika kuhimiza Uwazi na uwajibikaji katika mchakato wa bajeti. Pia ni mfano wa kuigwa kwa nchi nyingine.

Katika hatuba iliyotolewa tarehe 7 Desemba 2010 na kamishina wa bajeti bi Monica Mwamunyange alieleza kuwa maelezo yahusiayo bajeti kama mipango ya kati, matumizi ya bajeti, yanapatikana katika nyaraka mbalimbali kama taarifa ya mwanzo ya bajeti, mpango wa kati wa matumizi (Medium Term Expenditure Framework, taarifa ya utekelezaji ya MKUKUTA ([www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz)))

Tarehe 7 February 2011, Sikika ilitembelea tovuti tajwa na kutozikuta taarifa hizo za mwaka wafedha 2010/11. Hali hii inawanyima wananchi haki ya kufuatilia utekelezaji wa bajeti. na utendaji wake.

Pia Sikika imegundua ni kawaida kwa waheshimiwa wabunge kutopokea taarifa hizo katika muda muafaka. Kanuni za bunge toleo la 2007 ibara ya 96 inaeleza kuwa wabunge wanatakiwa kupokea vitabu vya makadirio ya bajeti siku 21 kabla bunge la bajeti kuketi.

Serikali inapaswa kuwapa mpango wa kati wa makadirio ya kila wizara kwa waheshimiwa wabunge. Ni katika makadirio ya kati ndiko kunakopatikana maelezo ya kina kuhusiana na matumizi ya kila wizara. Kwa kawaida vitabu vya bajeti hutoa maelezo kwa undani zaidi na ndipo wabunge wanaweza kupitisha bajeti ambayo hawajui kwa undani au isiyo na tija.

Kwa kuwasaidia wabunge kupitisha bajeti yenye tija kwa miaka ijayo tunaishauri serikali kuwapatia waheshimiwa wabunge vitabu vya bajeti siku 21 kabla ya kikao cha bajeti kuketi. Na kuwasaidia wananchi kufuatilia mazungumazo ya bajeti bungeni na kuwaelimisha wawakilishi wao tunaishauri serikali isiweke tu makadirio ya mwaka 2011/12 kwenye tovuti ya bunge baada ya Waziri wa Fedha kusoma Bajeti bali pia irahisishwe ili iweze kueleweka na yoyote atakayeweza kuisoma.

Baada ya kupitishwa kwa bajeti serikali inashauriwa kuiga kutoka katika nchi nyingine kama Uganda ambao wameanza kufankikisha kupatikana kwa vitabu vya bajeti kwa umma kwa kuweka taarifa hizo katika tovuti za serikali.

Mr. Irenei Kiria

Mkurugenzi Mkuu wa Sikika, P.O. Box 12183 Dar es Salaam,  
Tel: +255 222 666355/57, Fax: 2668015, Email: [info@sikika.or.tz](mailto:info@sikika.or.tz), Website: [www.sikika.or.tz](http://www.sikika.or.tz)